**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule 0754 627 501**

**Makamu Mkuu wa Shule 0684 202 063**

**Patron 0719 138 500 /0769 300 589 /0618 324 835**
**Shule ya Sekondari MWANDIGA**

**S.L.P 389**
**KIGOMA**

**Tarehe ……………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWANDIGA HALMASHAURI YA KIGOMA MKOA KIGOMA MWAKA …………………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……… na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **MWANDIGA** ipo umbali wa Kilometa 10 Kaskazini mwa Mji wa mkoa. Usafiri kutoka standi kuu ya basi Kigoma unapatikana kwa nauli ya Shilingi Tsh 3000/= kwa pikipiki na Shilingi Tsh 4000/= kwa bajaji. (kwa usafiri tu, kutoka standi kuu ya mabasi Kigoma wasiliana na mwl **0628 227 791/ 0756 710 382**)

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **...............**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **........................**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule





i. Sare ya shule hii ni suluali mbili rangi ya bluu kali (dark blue) zenye malinda matatu, upana chini iwe 16cm na iwe na turnup.

ii. Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu yenye ukosi (kola)

iii. Trucksuit moja ya kijani yenye mistari ya njano au unaweza kuipata shuleni kwa bei ya Tsh 20,000/=

iv. Sare ya Michezo (bukta ya bluu) na raba za michezo.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi nyeusi jozi mbili (au zaidi) za shule;

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta moja (1) rangi ya bluu shingo ya V

ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suluali mbili rangi nyeusi zenye malinda matatu, upana chini iwe 16cm na iwe na turnup.) na T- shirt moja ya kijani au unaweza kuipata shuleni kwa bei ya Tsh 12,000/=.

x. Tai mbili rangi ya bluu kali (ifanane na suluali)

xi. Tisheti moja rangi ya bluu bahari yenye nembo ya shule au unaweza kuipata shuleni kwa bei ya Tsh 15,000/=.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Kivuli (copy) ya cheti cha kuzaliwa, form four leaving na results slip.

ii. Madaftari 10 (counter book quire 3), au yanapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 3000/= kila moja.

iii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*rejea kiambatisho A*)

v. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology; au unaweza kuipata shuleni kwa bei ya Tsh 25,000/=

vi. Scientific Calculator fx 991, au unaweza kuipata shuleni kwa bei ya Tsh 35,000/=.

vii. Godoro futi 2.5 kwa 6, au unaweza kuipata shuleni kwa kulipia Tsh. 10,000/= kwa mwaka wa masomo.

viii. Mashuka Jozi 2 (rangi ya bluu /pink), blanket 1,

ix. Chandarua (Neti) 1, au unaweza kuipata shuleni kwa bei ya Tsh 8000/=.

x. Nguo za ndani za kutosha;

xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

xii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko; au zinapatikana shule kwa bei ya 5000/= kila moja .

xiii. Chombo maalumu cha maji ya kunywa (Galoni ya lita tano), au inapatikana shule kwa bei ya Tsh 1500/=.

xiv. Jembe 1 na mpini wake, mopper 1 na soft broom 1(mfagio wa ndani) kwa wanafunzi wa **PCB**

xv. Jembe 1 na mpini wake, squeezer 1 na hard broom 1 kwa wanafunzi wa **CBG.**

xvi. Jembe 1 na mpini wake , soft broom 1 (mfagio wa ndani) na mfagio 1 wa nje wenye mpini kwa wanafunzi wa PGM na PCM

xvii. Koti maalumu lenye rangi nyeupe la maabala (White laboratory coat) Kwa PCB, CBG, PCM and PGM

xviii. Bima ya afya (NHIF), Asiye na Bima aje na Tsh 50,400/= ili aombewe bima na shule kwa utaratibu maalumu.

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**ANGALIZO:**

Michango iliyoorozeshwa hapo juu ilipwe katika akaunti ya bank **NMB A/C 51601100067**. Jina la akaunti ni **MWANDIGA SEC SCHOOL**, Usisahau kuandika jina kamili la mwanafunzi aliyelipa michango juu ya pay slip ili kuweka kumbukumbu ya malipo afikapo shuleni. **Pesa hazitapokelewa mkononi.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba; Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa (line ya simu, vocha, charger) au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; **Rejea fomu No. 03**
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai; **Rejea fomu No. 01**
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; **Rejea fomu No. 02** na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu. **Rejea fomu No. 01**

**Kiambatisho A: vitabu**

Pamoja na vitabu vinvyopatikana shule, mwanafunzi kila somo husika anatakiwa kuja na vitabu vifuatavyo (**ANGALAU KILA KIMOJA KWENYE SOMO LAKE**)

| | |
|---|---|
| **Physics** | • S. Chand's principle of physics for class XI and XII<br>• Mastering physics part 1 and part 2<br>• abc modern physics part 1 and part 2<br>• Comprehensive_Physics JEE_Advanced_2016. |
| **Chemistry** | • Ramsden, E.N(2000) A' level chemistry<br>• S. Chand's principle of chemistry for class XI and XII |
| **Biology** | • Allison, L.A., Freeman, S., & Quillin, K. (2008). Biological science (5th Ed.). New York: Pearson Education.<br>• Campbell, N.A., Reece, J.B., Taylor, M.R., & Simon, E.J. (2005). Biology concepts and connections (5th Ed.). New York: Benjamin Cummings 1301 Sansome St. San Fransisco, CA 94111.<br>• Clegg, C.J. & Mackean D.G. (1994). Advanced biology, principles and applications (1st Ed.). London: John Murray (Publishers) Ltd. |
| **Advanced mathematics** | • Core cource mathematics<br>• Engineering mathematics 6th end – K.A. Stround |
| **Geography** | • D.T Msabila, physical geography<br>• Msabila human and ecomic geography<br>• Zisti Kamil, practical geography<br>• Zisti Kamil, physical geography. |
| **N:B** | **Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na mathematical set (mkebe) na rule** |

**SHULE YA SEKONDARI MWANDIGA**
**S.L.P 389**

**KIGOMA**

**FOMU NAMBA 01**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi …………………………………………………………………………
2. Jina la baba ……………………………………………………………………………
3. Jina la mama …………………………………………………………………………..
4. Jina kamili la mlezi ……………………………………………………………………
5. Anuani ya mzazi /mlezi ………………………………………………………………….
6. Uhusiano wa mlezi ……………………………………………………………………
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) ……………………………………
8. Kama ni mkulima zao mhimu analolitegemea ni ……………………………………….
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni ………………………………………………..
10. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni ……………………………………………………
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mleziaeleze wazi.
    ……………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………………………………………
    ……………………………………………………………
12. Madhehebu ya dini ………………………………………………………………………
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi

| Jina kamili | Kazi yake | Namba ya simu |
|---|---|---|
| (a) ……………………. | …………………. | ……………………… |
| | | PICHA |
| (b) ……………………………. | ……………………. | ................................ |
| | | PICHA |
| (c) ……………………………. | …………………….. | .............................. |
| | | PICHA |

**SHULE YA SEKONDARI MWANDIGA**
**S.L.P 389**
**KIGOMA**

**FOMU NAMBA 02**
**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA SHULE**

Jina la mwanafunzi ……………………………………………………………………………….

Jina la mzazi / mlezi ………………………………………………………………………………

Anuani ya mzazi /mlezi

……………………………………………………………………………

Uhusiano..............................................................................................(mjomba, shangazi, kaka, dada)

Mimi ……………………………………………………………… nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kulewa ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na naahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shule pamojana sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………………. Tarehe ……………………..

Mimi ……………………………………..……………… Mzazi / mlezi wa mwanafunzi ……………………..……………………………………………………… naahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi / mlezi wa mtoto huyu kwa kushirikiana na shule .

**SHULE YA SEKONDARI MWANDIGA**
**S.L.P 389**

**KIGOMA**

**FORM NUMBER 03**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To medical Officer 1/C of

………………………………………………………………

….......................Designated Hospital, P.O.BOX

……………………………………………………………………………….

Please examine the above named in full as to his /her physical and mental fitness for being able to pursue twoyears of Secondary School Education. The examination should include categories a-m

In case of any acute or defect / disability in each category or sub – category, may render the aspirant ineligibleof admission or eligible of admission to schools of a students with special needs.

(a) Student's name
………………………………………………………………………………
(b) Age
…………………………………………………………………………………………..
(c) Stool test
………………………………………………………………………………….
(d) Blood test
…………………………………………………………………………………
(e) Urine analysis
……………………………………………………………………………….
(f) Sphills test
…………………………………………………………………………………..
(g) Chest test
…………………………………………………………………………………
(h) Speech
……………………………………………………………………………………
(i) Eye test ………………………………………………………………………………..
(j) Abdomen ……………………………………………………………………………
(k) Chest X - ray …………………………………………………………………………….
(l) Sickle cell test
………………………………………………………………………………
(m) WCB total Differential ……………………………………………………………..

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule: SALUM KEAH MOHAMED**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

THE HEADMASTER
MWANDIGA SEC. SCHOOL
P. O. BOX 389
KIGOMA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754 627 501**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0684 202 063**
- **Mwandamizi Taaluma 0719 138 500**
- **Mwandamizi Malezi 0628 227 791**